VYDATE L GREEN KE 5L FLP K-35635.qxp 24/06/15 13:32 Page2


**MAELEZO KWA JUMLA**
VYDATE L ni dawa ya kuangamiza wadudu na viwavi na hufanya hivyo kwa kuingia kwenye mizizi, matawi na majani.
Dawa hii hutumika kuua viwavi *(Meloidogyne javanica)*, 'punk bud moth' na 'mealy bugs' ya mizizi kwenye nanasi. Vydate L hutumika pia kwenye waridi kuangamiza viwazi 'nematodes' wa aina ya *Meloidogyne spp.*

**JINSI YA KUTUMIA**

**Viwango na wakati wa kunyunyizia:** VYDATE L lazima itumiwe kwa njia ya aina ya unyunyizaji wa maji yanayo churuzika (*Drip irrigation)* kama ifuatavyo.

| MMEA | MDUDU | VIWANGO/ MUDA WA KUSUBIRI |
|---|---|---|
| Nanasi | Viwavi *(Meloidogyne javanica)* | Nyunyiza lita 10-12 kwa hektari kabla au punde tu baada ya kupanda na mimea kustawi.Halafu lita 10 kwa hektari kila baada ya siku 30. Muda wa kusubiri ni siku 30. |
| Waridi | Viwavi *(Meloidogyne spp.)* | Nyunyizia Lita 8-12 kwa Hektari. Nyunyizia viwango vya juu kwa mimea iliyostawi na iliy oathirika sana. AU Nyunyizia mara mbili (2) ukitumia Lita 6 kwa Hektari. Mara ya kwanza, wakati umepanda na mimea kushika. Mara ya pili ni baada ya mwezi mmoja (1) au miwili (2). Muda wa kusubiri ni Siku 2 kabla ya kuingia mahali palipo nyunyiziwa dawa isipokua umevalia nguo za kinga. |

**Kutayarisha Dawa:** Pima kiwango kinachopendekezwa cha VYDATE L na uchanganye kikamilifu na kiasi cha robo tatu cha maji yanayohitajika kwenye bomba la kunyunyizia huku ukiendelea kuongezea maji hadi kiwango kinachohitajika. Ili kupata matokeo bora , tumia vifaa vyenye uwezo wa kunyunyizia vya hali ya chini ~*(low pressure ground spray equipment)*.

**MADHARA/ TAHADHARI**
Dawa hii lazima itumiwe na mtaalamumwenye kujua matumizi yake. VYDATE L inaweza kudhuru inapomezwa au kupumuliwa. Epuka ukungu wa dawa unaponyunyizia na usinyunyizie moja kwa moja kwa wafanyi kazi wengine, wanyama au mifugo. Mahali unaponyunyizia dawa hii pasiwe na chochote au yayote asiye na hana mavazi ya kinga. Tenga wanyama na mifugo mbali na mahali umenyunyizia.

**Jinsi ya kutumia**
Vaa mavazi ya kinga kama vile 'overalls', kofia, 'gumboots', 'gloves', na vizuizi vya uso wakati unapoichanganya dawa na maji na unapoinyunyizia. Dawa hii ni SUMU inapopumuliwa , hudhuru inapomezwa , kuguza ngozi au macho. Usile, kunywa wala kuvuta sigara unapotumia dawa hii.

**Baada ya kunyunyizia**
Osha vizuizi vya mikono 'gloves' ukitimia sabuni na maji. Badilisha mavazi uliyokuwa umevaa na uoge kikamilifu mikono na ngozi iliyopatwa na dawa kabla ya kula, kunywa au kuvuta sigara.

**KUHIFADHI**
Hifadhi ndani ya chombo chake halisi kilichozibwa pahali pasipo na joto, pakavu na penye hewa safi ukiwa umeifungia mbali na watoto, madawa mengine, mbolea ama vyakula vya nyumbani au vya mifugo. usihifadhi ndani, au karibu na nyumba mnamoiishi watu au wanyama.

**KUTUPA VIWEKEO VILIVYOISHA DAWA**
Pasua na kuharibu kwa kivibondabonda vyombo vilivyoisha dawa na Kuvitupa mahali kuliko idhinishwa. Usivitumie vyombo vilivyo kuwa na dawa kwa kazi nyingine yoyote na kulingana na sheria za nchi za utupaji. Dawa iliyobaki pamoja na maji yaliyoosha chombo au bomba lazima yamwagwe kwenye shimo lililo mbali na visima au vidimbwi za maji na kulingana na sheria za nchi za utupaji.

**KUKINGA WANYAMA NA MAZINGARA**
1. Dawa hii ni sumu kwa samaki, ndege, na wanyama wengine. Usiinyinyizie moja kwa moja kwenye maji au kwenye mito, visima au vidimbwi za maji. Usichafue maji kwa kusafisha vyombo vilivyotumika kwa kutayarisha dawa hii, ama kumwaga maji yaliyo safishia dawa hii ovyo.
2. Dawa hii inaweza kuwadhuru nyuki ikinyunyiziwa moja kwa moja mahali walipo. Kwa hivyo usiitumie mahali nyuki walipo au pale wanapo pepea kutafuta nta. Itumie dawa hii wakati ambapo nyuki hawapatikani, au hawako kwa wingi.

**MAELEZO YA HUDUMA YA KWANZA**
**Ikiingia machoni:** Safisha macho na maji mengi kwa muda wa dakika kumi na tano ikiwa umefungua macho. Pata usaidizi wa daktari.
**Ikimwagikia ngozi:** Vua nguo zilizomwagikiwa na dawa mara moja na uoge kwa maji na sabuni. Kama ukitokwa na harahara ngozini, mwone daktari.
**Ikimezwa:** Ikiwa mgojwa yuko na fahamu, mpe maji mengi na kumfanya atapike kwa kuingiza kidole kwenye koo lake kwa utaratibu. Usimpe mgonjwa chochote kupitia kwa mdomo ikiwa amezirai. Mwone daktari mara moja apeane matibabu.
**Ikipumuliwa:** Muondoe mgonjwa na kumpeleka mahali penye hewa safi. Ikiwa hapumui, msaidie kwa kuongeza pumzi kwa mdomo. Mwone daktari mara moja.

**PELEKA MJERUHI KWA DAKTARI**
MAELEZO YA SUMU /ARIFA KWA DAKTARI

**Dalili za sumu**
Dawa hii ni Choline sterase inhibitor carbamate. Dalili za kusumika ni kama macho kupotea nguvu za kuona, Kuumwa na kichwa, kutokwa na jasho, kupumua kwa shida na kushikamana kwa misuli.

VYDATE L ni dawa aina ya *carbamate* ambayo huzuia 'cholinesterase'. Tumia dawa ya *Atropine Sulphate* kwa kiwango cha 1.2 - *2 mg* kwa shindano ya mishipa kwa muda wa kati ya dakika 15 – 30 ikiwa inahitajika. Dawa ya 2 – *PAM* inaweza kutumiwa ikiwa mgonjwa yuko ameathiriwa na VYDATE L pamoja na dawa aina ya *organophosphorous.* Usitumie dawa za *Morphine, Epinephrine* na *noradrenaline.*

**Wakati wa dharura piga simu bila malipo 0800 730030/0800 720021 (masaa 24).**

**ILANI KWA MTUMIAJI**
Dawa hii lazima itumiwe kulingana na maagizo yaliyo kwenye kibandiko. Ni hatia chini ya sheria za madawa ya kuangamiza wadudu waharibifu kutumia au kuhifadhi dawa hii katika hali isiyo salama.

**THIBITISHO**
Dhamana ya muuzaji ni maelezo yaliyo kwenye kibandiko ambayo ni lazima yafuatwe kikamilifu. Mnunuzi lazima akubali hatari zozote zinazoweza kutokea kutokana na matumizi ya dawa hii, kwenye binadamu au mali na lazima aikubali dawa hii katika hali hiyo.

BLACK